# Magonjwa yatokanayo na sigara

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kuna matatizo na magonjwa mengi na ya aina mbalimbali unayoweza kuyapata kutokana na utuvaji wa sigara. Kiungo rahisi kuathirika ni mapafu. Baada ya kuvuta huo moshi, kaboni na tindikali iliyomo kwenye tumbaku huishia kwenye mapafu. Malimbikizo haya ya kaboni na tindikali husababisha ugumu katika kupumua na kusabisha usaha kwenye mapafu. Matatizo haya ya mapafu humfanya mvutaji awe mwepesi kupata maambukizo mengine. Hii inaweza ikawa kikohozi sugu na pia inaweza kusababisha nimonia (kichomi) pamoja na kifua kikuu na sarakani. Nikotini vilevile ni mbaya kwa tumbo. Husababisha kupoteza hamu ya kula na maumivu katika sehemu za chini ya tumbo.

Unaweza ukaona kwamba wavutaji wakubwa wa sigara wakawa na meno meusi au machafu. Hii ni kwa sababu kaboni imejilimbikiza juu ya meno, na hivyo kubadilika kwa rangi. Watu wanaovuta mara kwa mara hutoa harufu mbaya mdomoni na hupata matatizo ya ngozi.